
# Báb

## *Mtangazaji wa Siku Mpya*




**Báb alizaliwa mnamo tarehe 20 Oktoba 1819 huko Shíráz, mji uliopo sehemu ya kusini ya Iran. Yeye alikuwa akingali mtoto mdogo, pale ambapo baba Yake alipofariki. Yeye alilelewa na mjomba wake, ambaye alimuweka shuleni kwenye umri mdogo.**




**Mwalimu wa Báb haraka alitambua uwezo wake mkuu na alielewa kwamba asingeweza kumfundisha mtoto asiye wa kawaida kama huyo. Báb alijaliwa na Mungu ujuzi wa asili.**



**Wakati ule watu wa Iran walikuwa wakingojea kuja kwa Mjumbe mpya wa Mungu. Waliomba kwamba Yeye angedhihirishwa mapema, na kuleta kipindi cha amani na haki juu ya ardhi. Wengi waliacha nyumba zao kumtafuta Mwahidiwa.**




**Mnamo jioni ya 23 Mei 1844, kijana mmoja aliwasili huko Shíráz akimtafuta Mwahidiwa. Báb alimkuta nje ya malango ya mji na alimkaribisha nyumbani kwake kujiburudisha baada ya safari yake ndefu. Hapo Báb alijitangaza kwamba Yeye alikuwa Yule Ambaye kuja kwake watu walikuwa wakingojea kwa shauku mno.**




**Neno “báb” maana yake “lango” au “mlango”. Báb alitangaza kwamba karibu Mjumbe mwingine wa Mungu angetokea ambaye angeunganisha watu wote wa ulimwenguni katika ukoo mmoja. Báb alikuwa kama mlango wa kuwaongoza wanadamu kwenye wakati ujao mpya na mtukufu.**



**Idadi ya wafuasi wa Báb iliongezeka kwa haraka. Kotekote Iran, wao walianza kuenezo mafundisho matakatifu ambayo Yeye Aliyafunuwa.**




**Lakini punde tu watu wa serikali na makuhani, ambao walikuwa wakiuogopa ukweli, waliinuka dhidi ya Imani hii mpya ya Mungu. Walimfunga Báb katika ng’ome katika sehemu ya mbali ya nchi, mbali kutoka kwa wafuasi wake.**



**Wafuasi wa Báb waliteswa kikatili sana. Walishambuliwa, walipigwa na kutupwa gerezani. Maelfu waliuawa, lakini Hoja ya Mungu iliendelea kuenea.**



**Katika mwaka 1850 Báb aliuawa kama shahidi. Kwa amri ya serikali, Yeye alitundikwa uwanjani pamoja na mmoja wa wafuasi Wake na alipigwa risasi na kikosi cha askari. Báb alikuwa mwenye umri wa miaka 31 tu.**



**Báb alitoa maisha Yake kuandaa njia kwa ujio wa Bahá'u'lláh, "Utukufu wa Mungu", Ambaye bendera Yake ya Imani ilikusudiwa kuinuliwa katika kila pembe ya dunia.**

Hakimiliki © 2021 ya Udhamini wa Ruhi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. Toleo la 2.1.1.PE.PV (tafsiri ya muda) Septemba 2023, zilizochapishwa katika kiswahili

Taasisi ya Ruhi
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org